# TARGETER KCPE JARIBIO LA TATU STAHIKI
## DARASA LA NANE - 2022

**STAHIKI- 003**

# KISWAHILI:
# SEHEMU YA KWANZA:
# LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40.**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI .**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali **1-50,** umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali: Chagua jibu sahihi.**

**18.** Tambua maneno yaliyopigiwa kistari

*Hebu nimtume mwanafunzi huyu, yule amekataa kabisa*

A. Kiashiria, kielezi, kiwakilishi.

B. Kionyeshi, kiunganishi, kielezi.

C. Kivumishi, kiwakilishi, kielezi.

D. Kielezi, kiashiria, takriri.

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

**16.** [A] [B] [C] [D] **17.** [A] [B] [C] [D] **18.** [A] [B] [C] [D] **19.** [A] [B] [C] [D]

**18,** kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja** tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

*Kimetayarishwa na kuratibiwa na taasisi ya uchapishaji ya Targeter Educational Publishers Ltd.*
*Email: info@targeterpublishers.co.ke*

**GEUZA UKURASA**

Scanned with CamScanner

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne.***

***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Bwana Mtindi hakujua kuwa___1___. Kila mwisho wa mwezi baada ya kupata___2___wake aliwazia pombe. Ilisemekana___3___sana___4___. Wakati wote wa heri, shari na fanaka au___5___hungemkosa magengeni___6___ pombe ya bei rahisi. Bwana huyu ilisemekana pia alikuwa na___7___ kwa kuwa hata aliweza kumwambukiza mke wake magonjwa ya zinaa.

1. A. kitu kilivunja mfupa na nguu kulala B. mali bila daftari hupotea bila habari C. cha mlevi huliwa na mgema D. kwenda bure si kukaa bure
2. A. fungule B. mshahara C. ada D. kifunguamkoba
3. A. alienzi B. alichukia C. alishuku D. alienziwa
4. A. kufanya bidii B. kulaza damu C. kula kikoa D. kupiga mtindi
5. A. uchungu B. sikitiko C. shauku D. ukosefu
6. A. yaliyouzwa B. zilizouzwa C. kulikouzwa D. yauzwayo
7. A. jicho la nje B. jicho la upekuzi C. jeraha la moyo D. kinyaa cha mambo

Vita___8___pombe haramu lazima___9___ kwa dhati yaani___10___ili jamaa kama Bwana Mtindi wakome___11___ pesa zao___12___ulevi. Bwana Mtindi lazima ajue kuondoa dari aezeke paa yaani; ___13___. Ni aibu ati hawawezi kupata___14___ ya shule kwa sababu pesa___15___ ulevini. Aibu!

8. A. dhidi ya B. juu ya C. licha ya D. baina ya
9. A. zipiganwe B. zipigwe C. ipiganwe D. vipiganwe
10. A. kwa hamu B. kwa ustadi C. kwa nia D. kwa uaminifu
11. A. kuvunja B. kufuja C. kuvuja D. kuvujilia
12. A. za B. na C. katika D. ya
13. A. watimize mambo yanayofaa kupendwa na wengi B. washughulikie mambo yanayowanufaisha wengi C. washughulikie mambo yanayofaa kupewa kipaumbele D. washughulikie mambo yenye umuhimu kwa wote
14. A. karo B. fola C. arshi D. ujira
15. A. lilitumika B. zilitumika C. vilitumika D. ilitumika



Scanned with CamScanner

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** Chagua jibu ambalo lina vihusishi pekee.

A. halafu, tena, yake, zote

B. ili, bali, wala, kama

C. mbali na, baina ya, bila, ama

D. karibu na, kando ya, katika, kuliko.

**17.** Tofauti ya maana kati ya matano na wa tano ni

A. watano ni idadi ya jumla na wa tano ni idadi kamili katika orodha

B. watano ni kuonyesha sifa na wa tano ni kuonyesha idadi

C. watano ni kuonyesha idadi kamili na wa tano ni anayechukua nafasi ya tano katika msururu.

D. watano ni idadi kamili na wa tano ni idadi katika msururu.

**18.** Ni sentensi ipi iliyotumia 'ki' ya udogo?

A. Kijiti hiki hakivunjiki rahisi.

B. Ukimpa hela hizo hatazifanyia kazi ya maana.

C. Kitoto chake hicho hakitulii darasani

D. Kiwavu ambacho kiliuawa kilikuwa kirembo.

**19.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi cha pekee.

A. Wanafunzi wale ndio wa shule yako, si hawa.

B. Sahani zote zilioshwa na nyingine zilihifadhiwa hivyo.

C. Gari lako ni jeusi nalo langu ni jeupe.

D. Ni mtoto pekee aliyeruhusiwa kuingia katika ukumbi huo.

**20.** Ni sentensi ipi kati ya hizi iliyo na kwa ya kifaa?

A. Fundi alikereza mbao kwa msumeno.

B. Kanisa lilitusaidia kwa siku arubaine.

C. Chifu aliwahimiza vijana kwa wazee kudumisha amani.

D. Wazee waliketi sako kwa bako wakiota moto.

**21.** Chagua kauli ya kutendewa ya sentensi hii:
*Juma aliandika kitabu akiwa kwa Rahab.*

A. Kitabu kiliandikiwa kwa Rahab na Juma.

B. Juma aliandikiwa kitabu akiwa kwa Rahab.

C. Kitabu kiliandikiwa Juma na Rahab kwake.

D. Juma aliandikiwa kitabu na Rahab kwake.

**22.** **Andika kwa wingi:**
*Baraza langu huongozwa na nahodha bahili.*

A. Baraza zetu huongozwa na manahodha mabahili.

B. Mabaraza yetu huongozwa na manahodha mabahili.

C. Mabaraza yangu huongozwa na nahodha bahili.

D. Mabaraza yetu huongozwa na manahodha bahili.

**23.** Chagua aina za maneno yaliyopigiwa kistari:
<u>Wale</u> ndio wapenzi <u>wakuu</u> na wanaenda <u>leo</u>.

A. Kivumishi, kielezi, kiwakilishi.

B. Kiwakilishi, kivumishi, kielezi.

C. Kiashiria, kielezi, kivumishi.

D. Kionyeshi, kivumishi, kielezi cha kutilia mkazo.

**24. Bainisha usemi wa taarifa wa:**

*"Ikiwa mnataka twende kwenu," alituambia Melisa, "ni lazima mngojee mama aje."*

A. Melisa alituambia kuwa iwapo tulitaka kwenda naye kwetu ingetubidi tungojee mama yake aje.

B. Melisa aliwaambia kuwa iwapo walikuwa wakitaka waende kwao ni lazima wangengojea mama afike.

C. Melisa alituambia kuwa ikiwa mnataka twende kwenu ni lazima mngojee mama aje.

D. Melisa alitaka kujua iwapo tungengojea mama aje ili twende naye kwetu.

**25. Tegua kitendawili kifuatacho:**

*Mwadhani naenda lakini siendi.*

A. Jua.

B. Mtoto.

C. Mvuli.

D. Mganga.

**26.** Arbuni ni

A. sehemu ya malipo ya kukopea kitu mwanzoni

B. sehemu ya fidia anayolipwa mtu mwanzoni

C. sehemu ya ujira wa kumsaidia mtu mwanzoni

D. sehemu ya bei ya kitu inayotolewa mwanzoni.

**27.** Wewe __________ uliyefunga bao la tatu.

Teacher.co.ke

A. ndiye

B. ndio

C. ndiwe

D. sio

**28.** Ni mpangilio upi ufaao kwa vifungu vifuatavyo ili kuleta maana kamili?

*(i) sharti lishughulikiwe*

*(ii) Uhifadhi wa mazingira*

*(iii) na kila mzalendo*

*(iv) ni jambo ambalo*

A. ii, iv, i, iii

B. i, iv, iii, ii

C. iii, iv, i, ii

D. ii, iii, i, iv

**29.** Ikiwa leo ni Alhamisi, mtondo itakuwa

A. Jumamosi

B. Jumapili

C. Jumatatu

D. Jumanne.

**30.** $\frac{8}{9}$ kwa maneno ni

A. tusui nane

B. thumni tidsa

C. sudusi nane

D. thumni tisa.



Scanned with CamScanner

**_Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40._**

Inasemekana kuwa hivi leo bara la Afrika lina takribani mataifa hamsini na manne. Bara hili lilitawaliwa na mataifa kutoka magharibi kabla ya kujinyakulia uhuru wake kuanzia miaka ya sitini. Wakoloni hawa walikuja kwa nia tofauti. Kuna wale walikuwa wakitafuta ubabe, wengine walitaka kupora mali yetu huku wengine wakidai kuwa walitaka kuleta mwangaza maadam waliliita bara letu kuwa bara la giza.

Leo hii bara la Afrika limebarikiwa kuwa na maliasili si haba. Kati ya maliasili hayo ni pamoja na misitu, miti, maziwa na hata mito. Aidha bara letu lina madini chungu nzima. Wataalamu wa madini waliwahi kunukuliwa wakisema kuwa ni karibu Afrika yote. Baadhi ya madini hayo ni pamoja na dhahabu, chokaa, chuma na hata mafuta.

Tuelewe kuwa madini huwa na faida chungu nzima katika bara letu na mabara mengine. Madini haya huiletea bara hili fedha za kigeni yanapouzwa. Fedha hizi hutumiwa katika kujenga na kuboresha miundomsingi katika bara hili. Yakini, yakinufaisha mataifa tajiri zaidi Afrika mathalan Afrika kusini, Nijeria, Misri na mengineo huwa na hazina kubwa ya madini'.

Ni wengi sana wamepata nafasi za ajira katika bara letu. Tuko na wataalamu wa kuchunguza mahali madini hupatikana. Wengine wengi nao hupata riziki yao kwa kuyachimba madini, wengine hujikimu kupitia usafirishaji wa madini hayo. Vilevile kuna mamilioni ya wafanyibiashara ambao wametajirika kupitia kwa msemo maarufu, 'Kuwa mkwasi kama muuza madini.

Najua utakubaliana nami kuwa katika maeneo ambayo madini huchimbwa huduma za kijamii huimarishwa. Maeneo hayo huwa na barabara nzuri, umeme na huduma za simu huwa za kisasa. **_Wakazi wa maeneo hayo hufaidika pakubwa kutokana na kugunduliwa kwa madini hayo_**.

Hata hivyo kama walivyosema wahenga, hakuna kapa lisilo na usubi. Licha ya faida hizi zote kochokocho za uchimbaji wa madini, pana changamoto tele zinazoambatana na uchimbaji huu. Kwanza mchimbaji huyu huchangia kwa kiwango kikubwa katika uchafuzi wa mazingira. Migodi huifanya ardhi kuwa chapwa na kutovutia kamwe. Halikadhalika, upasuaji wa miamba ya madini hueneza vumbi angani. Mavumbi haya hudhuru afya za watu na viumbe wengine. Uchunguzi uliofanywa mwaka wa 2017 na shirika la afya duniani ulidhihirisha kuwa asilimia kubwa ya watu wenye shida za macho na kifua ni wafanyao kazi migodini au walio karibu na migodi hiyo.

Hebu angalia machimbo mengi baada ya madini kupatikana. Machimbo haya hubaki wazi. Wakati wa msimu wa masika maji hujaa katika mashimo. Humo huwa ni mazingira bora ya mbu na wadudu hatari. Kuzaana kwa mbu hao hueneza ugonjwa wa malaria. Isitoshe, visa vingi vinazidi kuripotiwa na watu, hasa watoto, wanaotumbukia na kuzama katika vidimbwi vya machimbo ya migodi. Hata majambazi wengine kuwaua watu na kuwatupa kuko huko kwenye machimbo hayo.

Tuko pia na wapiga baruti zinazopasua miamba. Kando na kutoa sauti za kushtua watu sana hasa watoto na wenye msisimko wa damu baruti hizi hutikisa majumba yakajiporomokea. Madaktari husema kuwa sauti za baruti hizo zinaweza kumsababisha mtu uziwi asiweze kusikia tena. Hii ni kutokana na kuharibikiwa kwa viwambo vya masikio. Kumbuka. Masikio ya binadamu hayajaumbwa kuhimili sauti za hali ya juu.

Zaidi ya hayo wachimba migodi wengi hupoteza uhai wanapoanguka kwenye mashimo hayo ya migodi. **_Wakati mwingine machimbo hayo huporomoka na kumeza idadi kubwa ya watu kwa ulafi kama wa fisi_**. Machimbo mengine huwa zaidi ya kilomita ishirini kwenda chini. Hii ina maana kuwa kunao wachimba migodi ambao hukosa hewa safi ya okisijeni na kuaga dunia.

Changamoto kubwa ambayo hukumba nchi nyingi zilizo na utajiri mkubwa wa madini ni vita. Chukulia mfano kama vile Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo. Licha ya utajiri wake mkubwa wa madini, taifa hili limeishi kukumbwa na vita, ghasia, vurugu na machafuko ya mara kwa mara. Wakimbizi ni wengi sana katika nchi hiyo. Vita hivyo huenezwa na wakiritimba na mabepari ambao nia yao ni kupiganisha raia ili wao wenyewe wafaidhike kutokana na utajiri huo. Hata yapo mataifa mengine ya nchi za kigeni ambazo hufadhili makundi ya waasi kwa silaha na fedha ili serikali isiwe imara. **_Baadaye wanakuja kama wapatanishi huku wakipora madini ya nchi hiyo_**. Kutokana na haya madini badala ya kuwa baraka yanakuwa laana.

Uchimbaji madini pia hulemaza shughuli nyingine zote za uchumi. Unakuta wananchi wote wanataka kuchimba madini ilhali wako na mashamba ya kilimo. Njaa ikibisha hodi watu hawa hufa wakiwa na mashamba. Iwapo madini yataisha, watu hawa watakula nini?



Scanned with CamScanner

**31.** Inasemekana kuwa hivi leo bara la Afrika lina takribani mataifa hamsini na manne. Hii ina maana kuwa
A. bara la Afrika lina mataifa hamsini na manne
B. bara la Afrika lina zaidi ya mataifa hamsini na manne
C. bara la Afrika lina nchini ya mataifa hamsini na manne
D. bara la Afrika lina karibu mataifa hamsini na manne.

**32.** Wakoloni waliliita bara letu kuwa la giza kutokana na
A. ukweli kuwa halikuwa na maendeleo yoyote
B. ukweli kuwa bara la Afrika lina watu weusi
C. ukweli kuwa miti mingi hutumiwa kutengeneza makaa
D. ukweli kuwa wakoloni walitaka Waafrika peke yao wawe nchini Kenya.

**33.** Chagua jibu ambalo si sahihi kwa mujibu wa aya ya tatu.
A. Mataifa tajiri zaidi kama Afrika kusini huwa na madini mengi sana.
B. Madini huwa na faida chungu nzima katika bara la Afrika pekee.
C. Madini yanapouzwa nje ya nchi huiletea nchi fedha za kigeni.
D. Fedha zinazotokana na uuzaji wa madini hutumiwa katika kuboresha miundo msingi.

**34.** Ni methali gani mwafaka kuelezea kauli iliyopigiwa kistari?
***Wakazi wa maeneo hayo hufaidika pakubwa kutokana na kugunduliwa kwa madini hayo***
A. Hasira za mkizi faida kwa mvuvi.
B. Aliye juu mngojee chini.
C. Mgeni njoo mwenyeji apone.
D. Kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

**35.** Kulingana na aya ya tano ni wazi kuwa
A. maeneo kunakochimbwa madini huwa kuna kuboreshwa kwa huduma za maeneo hayo.
B. wakazi wa maeneo yanakopatikana madini hawafaidiki pakubwa kutokana na madini hayo.
C. madini hutoa nafasi nyingi za ajira kwa wakazi wa maeneo ambayo madini hayo hupatikana.
D. licha ya faida nyingi, madini huwa na madhara kwa watu wa maeneo yanakopatikana.

**36.** Uchimbaji wa madini kwa jumla
A. huwa na manufaa mengi sana na haina changamoto zozote zile
B. unafaa kuendelezwa katika maeneo ambayo hakuna watu wanaoishi huko
C. licha ya manufaa mengi kuna matatizo yake ambayo yanafaa kurekebisha
D. huwa na changamoto nyingi bila manufaa yoyote.

**37.** Taja tamathali mbili zinazojitokeza katika kauli ifuatayo:
***Wakati mwingine machimbo hayo huporomoka na kumeza idadi kubwa ya watu kwa ulafi kama wa fisi.***
A. Tashbihi, chuku
B. Tashhisi, kinaya
C. Kinaya, tashbihi
D. Tashhisi, tashbihi.

**38.** Zile baruti zinazotumiwa kupasulia miamba ya madini
A. huwashtua watu sana na kuwaua watu wengi
B. huathiri watoto na wenye maradhi ya msisimko wa damu licha ya kuharibu nyumba
C. huharibu viwambo vya masikio ya watu wote na kuwafanya kuwa za viziwi.
D. huchangia wachimbamigodi wengi kupoteza uhai wanapoanguka kwenye mashimo ya migodi.

**39.** ***Baadaye wanakuja kama wapatanishi huku wakipora madini ya nchi hiyo:***
Kauli hii inaonyesha watu hawa ni
A. wajanja
B. wanafiki
C. waongo
D. wajinga.

**40.** Gani haijatajwa kuwa athari mbaya inayotokana na uchimbaji wa madini?
A. Uchafuzi wa mazingira.
B. Matatizo ya kiafya.
C. Hatari za magonjwa.
D. Wanyama kuanguka machimboni.



Teacher.co.ke
Scanned with CamScanner

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Teacher.co.ke

Jua lilitua jioni hiyo. Tulikuwa tumeshinda mchana kutwa tukiendelea na masomo. Mwenyewe nilikuwa nimemwendea rafiki yangu anisaidie kutatua shida za hisabati ambazo zilikuwa zimenitatiza. Hatimaye tuliendelea na ziada. Palikuwa na utulivu na kimya kingi. ***Kusema kweli hata ungesikia kipande kidogo sana cha pamba kikianguka***. Utulivu huu ulitokana na ukweli kuwa tulikuwa tumeahidiwa mujarabu na zaidi ya yote mtihani mkuu ulikuwa ukibisha hodi.

Mara kimya kile kilikatizwa ghafla na milio iliyosikika kutoka nje. Zembe na mwenzake wakasikia kilio cha Moto!Moto!Moto! Kwanza tulifikiria ni udoto. Hata hivyo jinsi tulivyopuuza ndivyo sauti zilivyozidi kuhinikiza hewani. Zembe baada ya kukosa utulivu alifululiza nje ili kuona yale yaliyokuwa yakiendelea. Walipofungua mlango, wanafunzi waliona miale ya moto ikiwa karibu sana na darasa lao. Sote tukawa mguu niponye. Wanafunzi wenzangu waka bana mlangoni na madirishani. Walibanana kama ndizi kila mmoja akijaribu kujisalimisha. Kuna wale walioumia hapa na pale. Kwa bahati nzuri sote tuliweza kutoka kabla ya moto kulivamia darasa letu.

Nje zilikuwa ni hekaheka za kujaribu kuokoa maisha, majengo na mali. Punde si punde vikosi vya polisi na wazimamoto vikawasili. Polisi na utawala wa shule wakashughulikia kuwapeleka wanafunzi wote katika eneo lenye usalama. Wazimamoto na baadhi ya majirani wakawa na kibarua cha ziada cha kuzima moto ili usienee na kusababisha hasara kubwa. Malori ya wazimamoto nayo yakawa mbioni, huku ving'ora vikilia na kutahadharisha watu kuhusu hatari. Yakaleta maji ya kuzima moto baada ya muda wa bana na banua moto ulikuwa umezimika.

Kweli ujio wa wazimamoto ulirahisisha kuzimika kwa moto. Papo hapo ilifaa mambo ya dharura kufanywa. Kwanza tulihesabiwa. Ilidhihirika kuwa wanafunzi wawili hawakupatikana. Mwishowe ilidhihirika kuwa hawakuwa wamehudhuria masomo siku hiyo. Hata hivyo mabweni yalikuwa yamechomeka yote. Hivyo basi wanafunzi hawakuwa na pa kulala. Hata mali ya wanafunzi yaliangamia yote. Kuna baadhi ya wanafunzi ambao walizimia kutokana na kupumua moshi kwa wingi.

Kwa nyota ya jaha, shirika la msalaba mwekundu lilifika. Lilitoa huduma ya kwanza kwa wote waliozimia. Kama si shirika hili, wanafunzi wangelala nje wakizizimwa na baridi. Tulifurahia kuona kuwa tuliletewa mahema na kuundiwa makazi mapya. Kweli akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. Msaada wao ulinifaa sana mimi maadam nilikuwa nimeambiwa na daktari niepuke baridi.

Siku iliyofuata chanzo cha moto kilianza kutafutwa. Ilibainika kuwa, moto ulisababishwa na vijana waliotaka kurina asali ya mwalimu mkuu. Kumbuka hawakujua jinsi ya kurina kwa kuwa, baada ya kuvamiwa na nyuki walitoroka na kuacha moto ukiwaka. Moto ukaenea na kushika majengo jirani. Ulianzia ghala ya shule, ukaingia katika mabweni, maktaba na baadhi ya madarasa.

Kutokana na hasara kubwa, shule yetu haingeendeleza shughuli za masomo. Mwalimu mkuu ***alipiga kibirikizi*** kwa wazazi wote kuwa shule ingefungwa. Kufungwa huku kulidhamiriwa kuiwezesha serikali kuyajenga madarasa upya.



Scanned with CamScanner

**41.** Msimulizi alikuwa

A. akitatizwa na somo moja tu ambalo ni hisabati

B. na rafiki mmoja tu ambaye alikuwa gwiji katika somo la hisabati

C. na rafiki aliyekuwa wa msaada kwake

D. na mazoea ya kupuuza somo la hisabati.

**42.** Kwa mujibu wa aya ya kwanza,

A. wanafunzi walikuwa watulivu ili kusikiliza iwapo moto ungefika katika madarasa yao

B. wanafunzi walinyamaza kutokana na ukali wa mwalimu wa zamu

C. wanafunzi walitulia kwa matayarisho ya mitihani iliyokuwa mbele yao

D. utulivu wa wanafunzi ulitokana na ukali wa viranja wa darasa.

**43.** **<u>Heka heka</u>** ni

A. shughuli kadhaa zinazomletea mtu utulivu.

B. pilkapilka tele zinazomfanya mtu azubae

C. ghasia zinazosababishwa na adha fulani

D. shughuli nyingi zinazomfanya mtu asitulie.

**44.** Tulipogundua hatari iliyotukabili,

A. tulitoka nje ili kwenda kulala kabla ya kuchomeka

B. tulifunga milango na kuendelea na shughuli zetu za kazi

C. tuliacha kazi ya ziada na kukimbilia nje ili kuokoa maisha yetu

D. tulifungua milango na madirisha ili kupata hewa safi.

**45.** Ni tamathali gani ya lugha iliyotumiwa hapa?

***<u>Kusema kweli ungesikia kipande kidogo sana cha pamba kikianguka.</u>***

A. Kinaya.

B. Chuku

C. Tabaini.

D. Tashhisi

**46.** Wazo kuu linalojitokeza katika aya ya tatu ni kuwa

A. utangamano ni jambo aula wakati wa majanga

B. pesa ni kiungo thabiti wakati wa majanga ya mikasa ya moto

C. mazoezi ya kunyosha viungo ni muhimu wakati wa janga la moto

D. malori ni muhimu sana wakati shida ya moto inapobisha hodi.

**47.** Kifungu hiki kimedhihirisha wazi kuwa

A. ujuzi akali ni hatari sana na huweza kuleta hasara kubwa

B. wanafunzi wote walilimatia katika kupambana na moto

C. nyuki ndio waliosababisha moto uliochoma madarasa na mabweni ya wanafunzi

D. kurina asali ndicho kichocheo kikuu za moto wa shule nyingi.

**48.** ***<u>...alipiga kibirikizi</u>*** ina maana ya

A. aliwahatarisha

B. aliwatahadharisha

C. aliwakumbusha

D. aliwatangazia.

**49.** Uwajibikaji wa utawala wa shule unajitokeza pale

A. wanafunzi wote wanahamishiwa kwenye madarasa ya karibu

B. wanafunzi wanawaheshimu maafisa wa polisi katika eneo salama

C. walipowapigia wanafunzi simu wawaite wazazi wao

D. wanafunzi waliweza kuhamishwa na kupelekwa eneo salama.

**50.** Chagua methali mwafaka kuelezea hali hii:

***<u>Kweli ujio wa wazimamoto ulirahisisha kuzimika kwa moto.</u>***

A. Mgeni njoo mwenyeji apone.

B. Kaa akiinua gando mambo yamekatika.

C. Maji mengi hayazuiliki.

D. Maji moto hayaichomi nyumba.



Scanned with CamScanner